# THE SACRED NAME BROADCASTER

## Mtangazaji wa Jina Takatifu



12/2024

a publication of ***Assemblies of Yahweh***

# THE SACRED NAME BROADCASTER

*An **Assemblies of Yahweh** publication.*
***Assemblies of Yahweh**, **The Narrow Way Newsletter**, **The Sacred Name Broadcaster**, **The Sacred Name Broadcast**, **The Sacred Scriptures**, **The Sacred Name Telecast**, and **WMLK Radio** are Service Marks and Trademarks of Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507*

***December 2024***
***Volume LVI, Number 9***


# YALIYOMO



Page 1



Page 9



Page 18


**1** ***Messiah katika Agano la Kale, Sehemu ya 1 na 2***

*Ukristo unaamini kwamba Agano Jipya linajumuisha fundisho tofauti na Agano la Kale. Je, tunathibitishaje ukweli wa Messiah?*

**9** ***Viumbe vya Yahweh Vilivyoumbwa, Sehemu ya 1 na 2***

*Mwenye-enzi Yahweh aliumba aina nne za viumbe ili kumtumikia Yeye. Basi tuhakikishe kwamba hatulegei kamwe katika kujitolea kwetu kama walivyofanya wengine.*

**18** ***Sheria ya Yahweh: Amri ya Tisa, Usimshuhudie Jirani yako Uongo***

*Dekalojia inajumuisha uratibu wa Sheria za Yahweh na hujenga tabia ya kiroho ya kila mtu anayeweka maisha yake kwenye msingi huu thabiti.*



Mtangazaji wa Jina Takatifu huchapishwa kila mwezi na Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507. Uandikishaji wako umelipwa na watendakazi wenzi wenye hiari wa huduma hii ambao wanajali kwamba ujumbe huu wa wokovu unapaswa kutolewa bila malipo kwa ulimwengu wote kama shahidi kabla ya Ujio wa Pili wa Yahshua Masihi. Ingawa hakuna malipo yoyote yatakayotozwa kwenye chapisho hili, MICHANGO (yote inakatwa kodi) inakubaliwa kwa shukrani ili kusaidia kulipia gharama. Tunatumahi kuwa utashiriki katika kufanya habari hii ipatikane kwa wengine.

Nukuu zote katika The Sacred Name Broadcaster zimetolewa kwa The Sacred Scriptures, Bethel Edition, 1981, Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507, isipokuwa ikitangazwa vingenevyo. Tafsiri zote za Biblia humu, zimesahihishwa ziwe thabiti na maandishi yaliyo ya awali zaidi yanayopatikana. Nakala za The Sacred Scriptures, Bethl Edition, zinapatikana. Kwa ujumbe jinsi ya kununua kopi yako, andika kwa Assemblies of Yahweh.



© Hakimiliki 2024 Assemblies of Yahweh. Haki zote zimehifadhiwa.


Malipo ya posta ya mara kwa mara huko Reading, PA 19612 (ISSN 879320). Simu (717) 933-4518. POSTA: Tuma fomu 3579 kwa Assemblies of Yahweh, SLP C, Bethel, PA 19507.


***Mwanzilishi na Mwandishi:*** *Mzee Jacob O. Meyer*


## Jalada Letu

*Jalada la mwezi huu linaonyesha mitende katika En Gedi. Maji yanasafiri umbali mkubwa kupitia nyufa, au vipigo katika mawe mpaka yanapasua kwenye maporomoko mazuri ya maji.*

*Lazima tukumbuke daima jinsi Yahweh aliwatunza Israeli kwa miaka 40 nyikani. Yahweh aliwapa mana ya kila siku na kutoa maji kwa mawe. Kwa hivyo, kamwe tusisahau baraka ambazo Yahweh amemimina juu yetu kwa wingi sana.*

*Kusoma somo la maisha linatufunza kuwa lazima tuamini katika Yahweh wakati wote. Mara nyingi, tunategemea juu ya suluhu zetu badala ya kuamini katika Yahweh.*




***"Mtumaini Yahweh kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyoosha mapito yako. Usiwe mwenye hekima machoni pako; mche Yahweh, ukajiepushe na uovu. Itakuwa afya mwilini pako, na mafuta mifupani mwako."*** *(Mithali 3:5-8).*

*Daima Yahweh yupo kwa ajili yetu, kama mchungaji anayependa anayetunza kondoo Wake."Tufunze kuomba," wanafunzi wa Yahshua waliuliza, kwa sababu Yahshua aliweka mfano kwetu kuomba.* ***"Na yoyote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea."*** *(Mathayo 21:22).*

*Tunapokuwa katika hatarikatika uhitaji kwa mwongozo wa Yahweh, baraka Zake, au uponyaji Wake, kwa unyenyekevu uliza Yahweh kwa msaada, na atajibu kulingana na Mapenzi Yake.* ***"Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia...."*** *(1 Yohana 5:14).*



SEHEMU 1


# Messiah katika Agano la Kale

**Na Mzee Jacob O. Meyer**

Watu wengi sana wa kidini hawaelewi kwamba Biblia inajumuisha maagizo ya Baba wa Mbinguni yaliyotolewa kupitia muda wa miaka mingi, na kwamba kazi hii ya fasihi 66 tofauti kwa kweli inajumuisha kitabu kimoja kamili. Biblia inajumuisha kitengo kimoja kamili- zote Agano la kale na Mpya zimeunganishwa bila kutenganishwa kwenye juzuu moja. Lazima uelewe kwamba maneno ya Baba wa Mbinguni, yanayopatikana katika Maandishi ya Agano la Kale, kwa ukamilifu na kabisa yanaunda msingi wa Agano Jipya kwamba sehemu mbili za juzuu hili lililoongozwa zinakuwa kweli zisizoweza kutenganishwa. Mtu hawezi kugawa kati ya Agano la Kale na Jipya, au atafanya uharibifu kwa ujumbe mzima wa Biblia.

Watu leo wanaodhani kwamba Agano Jipya ni kitabu tofauti kabisa kutoka kwa Agano la Kale wako katika makosa. Agano Jipya linajumuisha uenezi wa baadaye wa ujumbe wa inayoitwa Agano la Kale. Kihistoria, Maandishi ya Agano Jipya yanatuambia kwamba Messiah alikuja duniani humu. Aliishi maisha ya haki, na kisha, akamwaga damu yake kwa ajili yetu kufidia dhambi zetu. Baada ya kifo chake na ufufuo, alipaa mbinguni ambapo anasubiri kazi leo kutoka kwa Mwenye-nguvu Yahweh Elohim, kurudi duniani kuanzisha Ufalme wa milele wa Yahweh.

Biblia kweli inaingiza jumbe hizi 66 kwenye juzuu moja kamili. Maandiko hayawezi kuvunjwa, Yahshua aliye Messiah alitoa maoni katika Yohana 10:35. Maandiko Matakatifu, kweli hayawezi kuvunjwa- katika Agano, kitabu, katika sura, katika mstari, au katika neno. Badala yake, shauri nzima la Yahweh linasimama kati-




ka umoja kamili kama lilivyofanya kwa zama. Haiwezi kuvunjwa, kupasuliwa, au kugawanywa, lakini lazima lisimame kama **kitengo kimoja kamili**. Vitabu vyake 66 kiishara vinawakilisha kamba za kinubi ambazo Mwabudu wa Kweli anapaswa kufanya wimbo wa usawa. Angalia Ufunuo 15:2.

Sasa, najiuliza kuwa hao wasomaji wanaoamini kwamba Agano Jipya ni kitabu tofauti kwa ukamilifu na kabisa kutoka kwa Agano la Kale, kama umewahi kuchunguza kwa uangalifu maandishi ya Agano Jipya na kutambua nukuu nyingi sana kutoka kwa maandishi ya Agano la Kale yanayopatikana hapo? Kulingana na takwimu fulani, kunazo nukuu 287 tofauti kutoka kwa Maandishi ya Agano la Kale zinazopatikana katika Agano Jipya; walakini, tunaamini kwamba , bila shaka, kuna mingi sana zinazotokea kama marejeleo ya kurudiwa au madokezo kwa nukuu za Agano la Kale.

Basi tuzingatie kitu fulani unawezakuwa umepuuzilia katika kusoma kwako kwa biblia. Yahshua aliye Messiah, anayesimama katika nafsi ya mtu wa kati katika Agano Jipya, tayari anawasilishwa katika nabii mingi za Agano la kale. Yahshua Messiah, aliyekuja duniani humu na kutembea njia ya maisha wakati anaingiliana miongoni mwa watu, ni mtu wa katikati wa Agano Jipya, wakati pia anaonekana kama mhusika wa katikati wa Agano la Kale.

Wakati Yahshua aliye Messiah alifufuliwa kutoka kaburini, alijitokeza mara kadhaa kwa wanafunzi Wake. Tunasoma kuhusu hili katika Luka mlango wa 24, kuanzia na mstari wa 44 kusoma chini hadi mstari wa 48. Katika kifungu hiki cha Maandiko, tungetaka kulipa kipaumbele maalum, kwa maneno haya ya Yahshua Messiah. Ni ya umuhimu sana.

***"Kisha akawambia, hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikiwa pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi. Ndipo akawafunua akili zao wapate kuyaelewa maandiko. Akawaambia ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Messiah atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanzia Yerusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya."***(Luka 24:44)

Yahshua aliye Messiah alipojitokeza kwa wanafunzi Wake, yeye Mwenyewe alileta kwa umakini wao, kwa nguvu sana, kwamba kuja Kwake duniani kulitabiriwa katika Maandiko Matakatifu. Messiah Mwenyewe alikuwa wa kupatikana katika maandishi ya Musa (Sheria [Torati] za Musa), Nabii, na Zaburi. Hizi ni sehemu tatu kuu za Biblia zinazoonekana katika inayoitwa Maandishi ya Agano la Kale- Sheria (Torati); Manabii (*Nebi'm*); na Zaburi (*Kethubim*). Kuchukua herufi ya kwanza ya kila moja ya maneno haya ya Kiebrania imetupa kifupi *TANAK*, ambacho Wayahudi wanaita Maandishi ya Agano la Kale- kwa maneno mengine, sheria za Musa, manabii wa Biblia, na fasihi za hekima. YAHSHUA ALIYE MESSIAH ALISEMA ALIKUWA WA KUPATIKANA KATIKA KILA MOJA YA SEHEMU HIZI ZA MAANDISHI YA AGANO LA KALE. Umetambua maoni haya na Yahshua aliye Messiah?

Kama Yahshua kweli ni mhusika wa katikati wa Agano la Kale, kwa nini wanathiolojia wanatupa Agano la Kale kiurahisi hivyo? Wanathiolojia wengi na wasomi

wanaamini kwamba Maandishi ya Agano la Kale yanapaswa kutupwa "juu ya lundo la takataka ya vizazi" pamoja na baadhi ya maandishi mengine ya kale, lakini inavyoonekana na kinyume chake, maandishi ya wanafalsafa wa Kigiriki yasifanyiwe hivyo. Sababu wanasisitiza kwa kufanya hili ni kwa sababu Maandishi ya Agano la Kale yanaamuru watu wa Aliye juu kudumisha haswa kiwango fulani cha maisha-kiwango cha juu cha maadili. Watu wachache sana leo wanataka kuambatana kwa kiwango hiki cha juu kimaadili.

Wanathiolojia wanajaribu kufikisha wazo kwamba kama mtu anaweza kuondoa Sheria, basi binadamu anaweza tu kufanya chochote anachopenda. Unaweza kuishi maisha yako hasa tu jinsi unavyotaka binafsi. Hakuna basi kujizuia, hakuna vikwazo vyovyote. Kweli, Biblia, maandishi ya Agano la Kale, yanaweka kiwango cha maadili. Kwa mfano, yanaonyesha mtu anayekufa nini ufafanuzi wa uzinzi. Inatangaza kwamba ushoga ni dhambi. Inasema pia, kwamba utaoaji mimba inajumuisha dhambi. Maandishi Matakatifu pia yanasema bila kutoridhishwa, kwamba siku moja kila wiki imeumbwa na kutengwa na Mwenye-nguvu kwa kusudi maalum; katika siku hii anataka watu Wake kutunza wakati takatifu kumheshimu Yeye na nguvu yake ya uumbaji kwa kusanyiko takatifu. Siku hiyo moja ya wiki (sabato ya siku ya saba) ni mwiba hivyo kwenye upande, kwa watu wengi ambao inavyoonekana wanataka kuondoa Agano la Kale nzima.

Watu wanapoanza kusoma Agano la Kale, linawalaani, kwa sababu linaonyesha wapi wanaishi katika makosa. Badala ya mabadiliko, kutubu na kubadilishwa, badala ya kujisalimisha mbele ya matakwa ya Aliye Juu Baba wa Mbinguni, wanatafuta njia rahisi kutoka mtanziko wao na kutafuta kuhesabiwa haki kwa kubatilishwa kwa sheria kupitia maandishi ya Mtume Paulo katika Agano Jipya. WAZO HILI LINAUNDA MAKOSA KUBWA YA KIMAFUNDISHO AMBAYO LAZIMA YAKATALIWE!

Biblia, Agano la Kale, inaongea kuhusu Yahshua Messiah. Inatuonyesha njia kwa maisha ya milele kama tu ifanyavyo Agano Jipya. Agano Jipya haiweki nje ujumbe tofauti kabisa kutoka kwa ule wa Agano la Kale. Agano Jipya ni uenezi wa baadaye wa Maandishi Matakatifu ya Kale kwa sababu yanathibitisha Agano la Kale. Agano Jipya kweli limejengwa juu ya msingi wa inayoitwa Agano la Kale.

Kwa hivyo, Yahshua aliye Messiah anajumuisha mtu mkuu kote kwa biblia, kuanzia na Mwanzo 3:15, ambapo imeandikwa kwamba mbegu ya mwanamke itaponda kichwa cha nyoka. Mbegu ya mwanamke, ikiashiria Messiah, ingemwangamiza nyoka, anayejulikana kama Shetani Ibilisi. Mkombozi Yahshua ataangamiza dhambi (wasio na sheria, angalia 1 Yohana 3:4), kuiondoa kuwepo milele. Hili hasa ndilo utume Wake ulikuwa alipokuwa hapa duniani. Alikuja kufidia kwa dhambi za binadamu kwa kuonekana kwake, na kufa kwa upatanisho wa dhambi zetu. Kweli Yahshua aliye Messiah ni mhusika wa katikati katika biblia, na lazima tumheshimu kwa hilo.

Rafiki kumbuka tu, tunapogeukia kwa 1 Wakorintho mlango wa 15, mlango wa ufufuo, Mtume Paulo anatangaza mawazo fulani ya kushangaza sana kama utabatilisha Agano la Kale. Paulo anasema,***"Basi ndugu, nawaarifu ile HABARI NJEMA niliyowahubiria; ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mnasimama, na kwa hiyo mnaokolewa; ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiria isipokuwa mliamini bure. Kwa maana niliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Messiah alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, KAMA KULINGANA NA MAANDIKO; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, KAMA YANENAVYO MAANDIKO."*** (1 Wakorintho 15:1-4).

Habari njema, kwa hivyo ni ya kupatikana imara katika Agano la Kale. Habari njema ya wokovu inajumuisha mafundisho kiini katika Agano la Kale, ikiwa na mizizi yake imewekwa imara katika dini ya Mwebrania-Mwisraeli- imani ya Kiebrania ya Ibrahimu, Isaka, na Yakobo- ikirudi nyuma hadi Mwanzo mlango wa 3, kufuata dhambi ya Adamu na Hawa.

Kwa nini Paulo anawaambia wasomaji wake kwamba aliwatangazia habari njema kulingana na Maandiko? Maandiko hayo LAZIMA, KWA LAZIMA, IWE Agano la Kale, Biblia ya Kiebrania, kwa sababu Agano Jipya lilikuwa wakati huo likiandikwa. Inawezekana kuwa tunaweza kusoma Agano la kale na kupata Yahshua aliye Messiah hapo, kama tu walivyofanya Kusanyiko la Kitume? Bila shaka, hili ndilo hitimisho pekee tunayoweza kufanya tunaposoma vifungu vya maandiko kama hivi. Kwa kweli vipi tunaweza kuthibitisha kwamba Yahshua aliye Messiah ni Messiah wa kweli bila maelezo yake ya msingi katika Agano la Kale?

Mtume Paulo, na Kusanyiko la Kimitume la Agano Jipya wote walipata mizizi yao katika Agano la Kale, na wewe na mimi pia lazima tufanye vivyo hivyo leo.

Kwa sababu hiyo, ninaanza mfululizo wa jumbe kuhusu Messiah katika Agano la Kale. Ungana

nasi kila mwezi kwa chapisho la sehemu mpya ya mfululizo huu.

Biblia lazima iwe ya kutumika kwa kila mtu binafsi. Tumegundua kwamba unabii wa Biblia unaleta ujumbe wa kimaandiko hadi nyumbani kwetu.

Yahshua aliye Messiah katika Agano la Kale anawakilisha kipengele kikubwa cha unabii wa kimaandiko.


Kama hujawahi kusoma unabii wa Biblia kuelewa matukio yanayokuja mbele yetu, basi nakuhimiza kusoma kila toleo la jarida la **The Sacred Name Broadcaster** kwa makini na kutambua jinsi hii kweli linafanya ujumbe wa Biblia wa kutumika kwa kila mmoja wetu leo.

Woga wa isiyojulikana unasababisha wasiwasi, hata hivyo, unapojua nini iko mbele, kwa ujasiri utajua jinsi ya kujitayarisha vyema kukutana nayo.

Kumbuka onyo ambalo Mtume Petro ametoa kwetu kuhusiana na maandishi ya Paulo. ***"Kwa hiyo wapenzi, kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake. Nanyi uhesabuni uvumulivu wa Mkuu wetu kuwa ni wokovu, KAMA VILE NA NDUGU YETU MPENZI PAULO ALIVYOWAANDIKIA KWA HEKIMA ALIYOPEWA; VILE VILE KAMA KATIKA NYARAKA ZAKE ZOTE PIA, AKITOA HUMO HABARI ZA MAMBO HAYO; KATIKA NYARAKA HIZO YAMO MAMBO AMBAYO NI VIGUMU KUELEWA NAYO, NA MAMBO HAYO WATU WASIO NA ELIMU, WASIO IMARA, HUYAPOTOA, KAMA VILE WAYAPOTOAVYO NA MAANDIKO MENGINE, KWA UVUNJIFU WAO WENYEWE. Basi, wapenzi mkitangulia kujua hayo, jilindeni nafsi zenu, msije mkachukuliwa na kosa la hao wahalifu mkaanguka na kuuacha uthibitifu wenu. Lakini, kueni katika neema, na katika kumjua Mkuu wetu na Mwokozi Yahshua Messiah...."*** (2 Petro 3:14-18a).

Lazima tuhitimishe kwamba Paulo hangebuni mafundisho yanayopingana na amri za Agano la Kale, hata ingawa maandishi yake wakati mwingine yanaonekana yenye utata. Kwa kujua Agano la Kale, tunaweza kuyaelezea SAHIHI. Mtume Petro ameonya Waabudu wa Kweli wasiwe wahasiriwa kwa uharibifu ambao Paulo dhahiri hakunuia kuleta kwa watu wa Yahweh.

Basi na tusikie nini aliandika katika 1 Wakorinthο 7:19 : ***"Kutahiriwa si kitu, na kutokutahiriwa si kitu bali kuzihifadhi amri za Yahweh***[ni kila kitu]***."*** Ujumbe huu ni wazi kweli kote katika Biblia! Utaukubali? SNB



***Linapatikana kwenye Mlima uliofichwa magharibi mwa Los Lunas, New Mexico, Jiwe la Dekalojia ni mchongo kwenye jiwe kubwa la Amri Kumi kwa kutumia maandishi ya kale ya Kiebrania.***



Na Mzee Jacob O. Meyer

# Messiah katika Agano la Kale

## SEHEMU YA 2

Mara moja baada ya ufufuo, Yahshua aliye Messiah alifanya jambo la ajabu sana. Kama anawaelekeza wanafunzi wake katika Luka mlango wa 24 (kuanzia kusoma mstari 44), alifanya kauli ya ajabu na muhimu ambayo inapaswa kushtua wengi sana wa watu wenye dini.

Basi tusome maneno yake mwenyewe. ***"Kisha akawambia, hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa ningali pamoja nanyi, YA KWAMBA NI LAZIMA YATIMIZWE YOTE yaliyoandikwa KATIKA TORATI YA MUSA, na katika MANABII na ZABURI. Ndipo akawafunua akili zao wapate kuyaelewa maandiko. Akawaambia ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Messiah atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanzia Yerusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya."***

Katika kifungu hiki cha kipekee cha Maandishi, Yahshua aliye Messiah kwa nguvu alikuwa amejitolea Mwenyewe kwa ukweli kwamba alikuwa kweli utimilifu wa nabii za kimessiah za Maandishi ya Agano la Kale. Kwa nguvu alisisitiza ukweli huu muhimu: kwamba maisha yake ya dunia ni utimizaji wa mambo yote yaliyoandikwa **katika sheria ya Musa** na manabii na Zaburi kutimizwa na Messiah. Alionyesha kuwa alikuwa pia mwigizaji mkuu- mtu mkuu- wa Agano la Kale, Biblia ya Kiebrania, kama tu hakika alivyo mhusika mkuu wa Agano Jipya.


Ukweli unaobainisha kuhusu Andiko hili, unapozingatia kwa uangalifu, unathibitisha kwamba ujumbe wa Biblia hauwezi kuvunjwa, kugawanywa au kutengwa, katika Maagano! Wengi wa ukristo wa kawaida leo wanaamini na kufunza kwamba Agano Jipya linajumuisha juzuu tofauti kabisa kuliko Agano la Kale, lakini sote tunajua kwamba hitimisho hili sio la kweli. Linaloitwa Agano Jipya, kweli, haliwezi kutenganishwa na Agano la Kale.

Kunazo nukuu nyingi kutoka Agano la Kale zinazopatikana katika Maandishi ya Agano Jipya, na mingi ya nukuu hizo zinahusiana kwa maisha na huduma ya Yahshua aliye Messiah. Unabii wa kwanza wa Yahshua aliye Messiah unapatikana mapema kama Mwanzo 3:15, ambapo tunaambiwa kwamba mbegu ya mwanamke inatabiriwa kuponda kichwa cha nyoka. Mbegu ya mwanamke inaashiria Messiah, na kichwa cha nyoka kinaelekeza kwa Shetani Ibilisi, Mjaribu ambaye aliwashawishi Adamu na Hawa kwa ujanja kufanya dhambi.

Adui Shetani alitoa ushawishi wake juu ya Adamu na Hawa, kuwashawishi kufanya dhambi na kuasi dhidi ya amri za Mwenyenguvu Yahweh. Kwa hivyo, kutoka wakati huo, waliwekwa chini ya hukumu ya kifo na Mwenye-nguvu Yahweh. Adamu na Hawa walikataliwa na kuendeshwa kutoka Paradiso, bustani ya Edeni na Mwenye-nguvu Yahweh; walakini, walikuwa na fursa kuangalia mbele kwa sadaka ya upatanisho ya Messiah. Wangeangalia mbele kwa wakati Messiah angekuja duniani humu na kufa kwa dhambi za binadamu kupanua msamaha Wake kwa unyanyapaa wa dhambi ambao ungepitishwa kama udhaifu wa tabia kwa kizazi chao.

Yahshua aliye Messiah kweli ni mhusika mkuu wa Biblia, kuanzia nyuma kabisa katika Mwanzo 3:15. Ndiye Mbegu iliyoahidiwa, ambaye aliteuliwa kukomboa kutoka kwa dhambi kizazi kilichotubu cha familia ya Adamu na Hawa. Kabila ya binadamu ilipewa mpango wa wokovu na Mkombozi katika Mwana wa Yahweh- Yahshua.

Yahshua aliye Messiah kweli alitimiza Maandishi haya ya




kinabii,lakini wanafunzi hawakuweza kuelewa zote za tabiri hizi. Yahshua aliye Messiah alifungua kuelewa kwao ili waweze kuelewa nabii hizi za Maandiko. Alifungua akili zao na nyoyo ili kwamba wangeweza kuelewa nabii za Maandiko zilizorejelea kwa Yahshua aliye Messiah Mwenyewe na kuelezea utume Wake kama Messiah.

Wakristo wengi wa kawaida katika wakati wetu wanaamini kwamba Mtume Paulo pengine alianzisha dini mpya ya Ukristo. Wanaamini kwamba wakati wanapotenganisha kati ya maandishi ya Agano la Kale na Jipya, mtu atapata aina tofauti ya dini katika Agano Jipya kuliko nini inafundishwa katika Agano la Kale. Wanasisitiza, kuthibitisha na kudai kwamba huu ndio ujumbe ulio na Biblia. Lakini mawazo haya yako katika makosa!

Mtume Paulo alihubiri fundisho katika maelewano kamili na wanafunzi wengine. Bila shaka utakumbuka kifungu katika Wagalatia mlango wa 1, ambapo alisema kwamba hakuhubiri ujumbe mwingine, au tofauti, kwamba baada ya uongofu wake, kwa bidii alisoma Biblia akiwa Arabia kwa muda fulani. Miaka mitatu baadaye, alipanda Yerusalemu, alipozungumza na Mtume Kefa kuamua kama ufahamu wake wa mafundisho ya kimessiah ulikuwa sawa kabisa kama uliohubiriwa na Mitume. Alipata kwamba wote, yeye na mitume wengine kweli walihubiri kabisa ujumbe sawa, na kwamba hakukuwa na kutokubaliana kati yao wa mafundisho. Nini ilikuwa sababu? Jibu ni kwamba walikuwa wote wakihubiri kutoka kwa maandishi ya Agano la Kale. Kutokubaliana kati yao kulichipuka baadaye.

Hata hivyo, bado Paulo alihubiri, na kuendelea kufunza, hasa ujumbe sawa (habari njema ya wokovu) ambayo ilikuwa ikifundishwa na Mitume wengine, iliyofanana kama alivyokuwa Yahshua kote katika huduma, kote hadi mwisho kabisa.

Umewahi kusoma 2 Petero 3:15-16? Kifungu hiki katika Agano jipya, kilichoandikwa na Mtume Petero, kinaelezea Paulo kama mwandishi ambaye anaelewaka vibaya sana. Wakati mwingi ninapoandika nakala au tahariri kwa jarida la **The Sacred Name Broadcaster**, najiuliza jinsi mtu mwingine ambaye atasoma maandishi haya, atayaelewa, kuyatafsiri, au kuitikia kwa ninachoandika. Kama ninazungumza hewani, nikitafuta kuuwambia ulimwengu mzima kuhusu Ukweli wa Mwenye-nguvu Yahweh na Ukweli wa Maandishi yaliyoongozwa, najiuliza nani ambaye angekuwa katika hadhira inayosikiliza na hasa jinsi wanaelewa ninayosema.

Pengine wasomaji au wasikilizaji wanaweza *kuelewa vibaya* ninachosema. Pengine wangekuwa wa kuwashwa kwa tofauti katika mafundisho ambayo wamezoea kusikia na karibuni kufunga **The Sacred name Broadcast**. Hata hivyo, sipangi kusema chochote ambacho makusudi kitamkasiri-

sha yeyote, lakini bila woga au kutoridhishwa, ninanuia kuhubiri Neno safi la Yahweh. Pengine, kama watu wanasoma vitu fulani katika jarida la **The Sacred Name Broadcaster**, wangechukua utafsiri mbaya kutoka kwa yale maandishi yetu yanafunza, lakini tunapanga kuchapisha tu mafundisho safi ya Yahweh. Tunazungumza bila woga.

Kwa sababu hiyo, **The Sacred Name Radio Broadcast** na jarida la **The Sacred Name Broadcaster** zinatumwa kwa maombi yetu katika tumaini kwamba watu watakubali nini tunahubiri na kuchapisha katika njia ya moja kwa moja. Usichukue neno letu kwa chochote tunafunza, badaia yake, chukua Biblia yako mkononi na kujiangalilia mwenyewe nini Biblia inasema kwa mada hizi za kimaandiko.

Ni wazi Paulo alikuwa mtu aliyeleweka vibaya sana. Petro anasema kwamba alikuwa hata KWA MAKUSUDI kutoeleweka. Basi tusome 2 Petro 3:15-16, ***"Nanyi uhesabuni uvumulivu wa Mkuu wetu kuwa ni wokovu, kama vile na ndugu yetu mpenzi Paulo alivyowaandikia kwa hekima aliyopewa; vile vile kama katika nyaraka zake zote pia, akitoa humo habari za mambo hayo; katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo, na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, kama vile wayapotoavyo na maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe."***

Baadhi ya watu ambao wasiojifunza na wasio imara kwa Mandiko ya Agano la Kale, inavyoonekana wanapotosha alichoandika Mtume Paulo katika jumbe alizotuma katika nyaraka zake, anaonyesha Mtume Petro.

Ni ya kushangaza kwamba badala ya kuruhu Agano la Kale kuzungumza kwa nguvu kama kiini hasa na msingi thabiti wa imani yetu, watu wengi katika Ukristo wa kawaida wameitupa! Watu wengi leo wanaamini kwamba Maandishi ya Agano la Kale yanapaswa kutupwa juu ya "lundo la takataka za zama," pamoja na baadhi ya maandishi mengine ya kale.

Hiki ni kitendawili gani! Sivyo kesi ilivyo. Agano Jipya ni, kwa kweli, uenezi tu wa baadaye na unaotegemea kabisa juu ya maadishi ya Agano la Kale. Agano la Kale linaunda msingi wa Imani yetu. Linayo Sheria iliyoundwa na Mwenye-nguvu Yahweh kutoa kiwango thabiti cha maadili kuelekeza watu wa Aliye Juu kuelekea Ufalme Wake. Inatabiri kuhusu Messiah na zama zijazo.

Basi tuangalie kwa anayosema Mtume Paulo katika 1 Wakorintho 15. ***"Basi ndugu, nawaarifu ile habari njema niliyowahubiria; ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mnasimama, na kwa hiyo mnaokolewa; ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiria isipokuwa mliamini bure. Kwa maana niliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Messiah alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kulingana na maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko."***(1 Wakorintho 15:1-4)

Hapa, Mtume Paulo, kama anaandika alithibitisha mateso, kifo na ufufuo wa Yahshua aliye Messiah kwa Kusanyiko la Wakorintho moja kwa moja kutoka kwa Maandishi ya Agano la Kale. Lazima iwe Maandishi ya Agano la kale aliyotumia kufanya hili, kwa sababu Agano Jipya lilikuwa wakati huo likiandikwa. Paulo anaonyesha kwamba habari njema hii inapatikana katika Agano la Kale. Istilahi *habari njema* kama inavyoonekana katika **King James Version**, ni *gospel*, lakini hilo sio neno nzuri kutafsiri neno la Kigiriki **euaggelion**. Neno hili la Kigiriki (linapotoka neno la Kiingereza *Evangel*) linamaanisha *habari njema*. Habari hiyo njema ni mpango wa wokovu unaopatikana katika Maandishi ya Agano la Kale, kama anavyothibitisha Paulo!

Tunaweza kufungua kurasa za Maandishi ya Agano la Kale, na tunaweza kugundua nabii za Messiah kote kwenye juzuu. Utabiri wa Yahshua Messiah na utume Wake uko hapa kutoka Mwanzo hadi Malaki, na hilo ndilo linafanya Biblia ya kipekee hivyo na

***Tunaweza kufungua kurasa za Maandishi ya Agano la Kale, na tunaweza kugundua nabii za Messiah kote kwenye juzuu. Utabiri wa Yahshua Messiah na utume Wake uko hapa kutoka Mwanzo hadi Malaki, na hilo ndilo linaifanya Biblia ya kipekee hivyo na ya kuvutia.***

ya kuvutia.

Biblia zaidi inajumuisha kitengo cha mshikamano kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Hauwezi kutenganisha Biblia kwenye vitengo- **haiwezekani**! Hauwezi kuitenganisha katika Maagano, au kwa vitabu kutoka kwa 65 zilizobaki. Hauwezi kutoa mlango nje ya muktadha, kuidondoa kutoka kwa kitabu na kujenga kesi ya kimafundisho juu yake, wala yeyote hawezi kutoa mstari, au neno, na hivyo kutenganisha fundisho kutoka kwa mafundisho yaliyobaki ya biblia. Biblia nzima-vitabu vyote 66- inashikilia imara pamoja kitengo kimoja, kufundisha fundisho moja la umoja na safi.

Naamini kwamba utaungana mara kwa mara kama tunatafiti Neno la Yahweh, na tutaona katika vitengo vinavyokuja jinsi Messiah anapatikana katika Maandishi ya Agano la Kale. Sikiliza mara kwa mara kwa **The Sacred Name Broadcaster** na kusoma Maandiko Matakatifu na msaada wa **The Sacred Name Broadcaster** na maandishi yetu yaliyochapishwa. Kamwe hautajutia! Utajifunza mingi ya kweli kila siku. SNB

# *Assemblies of Yahweh*

## Taarifa ya Mafundisho Pointi #3

### Tunathibitisha

- Kwamba Messiah amekuja kwa mwili wa ubinadamu kama mtu aliyetambulika kama Mwokozi katika Maandiko ya Agano Jipya.
- Na ya kuwa awali alikuwapo (pre-existed) na Baba. Yohana 16:28-30; Zaburi 2; Mika 5:2; Yohana 17:5; Filipo 2:5-8
- Na kwamba alizaliwa na bikira, Mathayo 1:18, 23; Luka 1:26-38.
- Na kwamba Yeye aliishi maisha yasiyo na dhambi, 1 Petero 2:22
- Ili kupitia kifo chake juu ya mti wa Kalvari tunaweza kuwa na upatanisho (atonement) kwa ajili ya dhambi zetu, Isaya 53; Waebrania 9
- Na kwamba alifufuka siku ya tatu, Mathayo 12:40; 1 Wakorintho 15:1-8
- Ili pia nasi atupe tumaini la ufufuo, Warumi 5:6-12, 1 Yohana 5:9-13.
- 
- 



# Viumbe vya Yahweh Vilivyoumbwa

SEHEMU YA 1 & 2

**Na Mzee Jacob O. Meyer**

Umewahi kuzingatia wingi halisi wa mada zinazojadiliwa kwenye Biblia? Biblia inazo nyenzo zinazohusu mada nyingi. Katika awamu zijazo kadhaa zinazoshirikiana na nakala yetu ya matangazo ya redio, ruhusu tujihusishe na utafiti wa somo linalohusiana na darasa nne za viumbe vilivyoumbwa ambavyo viliumbwa na Mwenye-nguvu Elohim, Aliye na Nguvu wetu Yahweh, ili kumtumikia yeye.

Mwenye-nguvu Yahweh ameumba binadamu katika sura yake mwenyewe; walakini, hilo halina maana kwamba uwepo wa mtu ni kama Yahweh(ambaye ni roho). Mtu aliumbwa nafsi hai, yeye hana nafsi.Lazima tuzingatie, walakini kwamba mtu ana roho ndani yake, ambayo inaitwa pumzi za uhai. Neno la Kiebrania ni *neshamah*. Inapaswa pia kutajwa kwamba binadamu anaweza kupewa Roho Mtakatifu, unaitwa katika Kiebrania *ruach hakodesh* (Roho Mtakatifu). Roho Mtakatifu ambao anatoa kwa watumishi Wake watiifu hatimaye utamwongoza mtu katika kuwa mtumishi mnyenyekevu wa Yahweh Elohim na Mwana Wake, Yahshua.

Katika utafiti huu, pia tutazingatia viumbe mbalimbali ambavyo Mwenye-nguvu Yahweh ameumba kuwa katika huduma Yake maalum. Tunaweza kusoma kuhusu uumbaji wa binadamu katika Zaburi 8. Tunasoma hapo kwamba mtu amepewa wajibu wa kutunza Uumbaji wa Yahweh-dunia hii- na vyote vilivyomo. Zaburi 8, kuanzia mstari wa 4, inasoma, ***"Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na binadamu hata umwangalie? Umemfanya mdogo punde kuliko Elohim, Umemvika taji ya utukufu na heshima.Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; umevitia vitu vyote chini ya miguu yake...."***

Mwandishi, Mfalme Daudi basi anaendelea kuorodhesha "vitu vyote" Yahweh ameweka chini ya miguu ya binadamu, wanyama, ndege, na samaki wa baharini. ***"Wewe, Yahweh, Mfalme wetu jinsi lilivyo tukufu jina lako duniani mwote!"*** Ni mshangao wa furaha katika kutambua Jina la Yahweh.

Umuhimu wa Jina la Yahweh tena umeonyeshwa hapa katika Zaburi hii, kama Jina la Yahweh linaonekana mara nyingi hivyo katika Biblia. Kwa kweli, neno "Jina" linaonekana kwa wastani karibu mara moja kwa kila ukurasa kwenye Biblia! Jina la Mwenye-nguvu Yahweh ni lenye maana zaidi na muhimu, kwani linatumika mara kwa mara, haswa katika Zaburi, likionekana mara 6,823 katika Agano la Kale. Kunayo pia matukio ya ziada ambayo liliondolewa.

Ruhusu tuzingatie swali hili kwa sasa: "***Mtu ni kitu gani?"*** Neno lililotafsiriwa mtu ni *enosh* katika maandishi ya Kiebrania, na linamaanisha *mtu katika udhaifu wake wote*. "***Au Mwanadamu...."*** Neno hili katika maandishi ya Kiebrania linaonekana kama *ben adam*. Adamu linatumika katika Mwanzo kwanza kama neno la jumla kwa binadamu (Yahweh aliumba Adamu [mtu au binadamu]). Baadaye, jina Adamu linatolewa kwa mtu wa kwanza mwanamume ambaye Yahweh aliumba, na kwa hivyo, linakuwa NOMINO SAHIHI. Bibi yake, aliyeumbwa kwa ajili yake, aliitwa *chawah* au kama watafsiri wa Kiingereza wanalitoa, *Eve*.

Pia, kwa kuongezea, kunazo darasa tatu, za viumbe walioumbwa ambao lazima wazingatiwe kando ya binadamu. Hawa ni viumbe wa kiroho wanaoitwa kwa kawaida malaika, makerubi, na maserafi. Kwanza, tutazingatia neno *makerubi*.Mara ya kwanza ambapo neno hili linaonekana inapatikana katika Mwanzo 3. Wakati Adamu na Hawa walitenda dhambi, Mwenye-nguvu Yahweh aliwaendesha nje ya paradiso yake nzuri, ambayo ni shamba la Edeni, shamba la furaha ya ajabu, bustani kamilifu ambalo alipanda, au kama katika maandishi ya kiebrania *gan Eden*.

Tunaambiwa katika Mwanzo 3:22 kwa nini Yahweh Elohim ilibidi awaondoe nje ***"Yahweh Elohim akasema, Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya; na sasa asije akanyosha mkono wake akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele; kwa hiyo Yahweh Elohim akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa. Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima."***

Neno *makerubi* linaloonekana katika maandishi ni kutoka kwa neno la Kiebrania ambalo ni la toleo lisilo na hakika. Linaonekana katika umbo la wingi wa kiume wa *cheruv*, ambalo ni #3742 katika **Strong's Exhaustive Concordance Hebrew Dictionary**. Makerubi hawa (mwisho wa wingi wa kiume) wamewekwa kama walinzi kiingilio mwa Bustani ya Edeni, kuhakikisha kuwa binadamu hawezi kurudi. Kuongezea, Yahweh aliweka hapo upanga wa moto unaogeuka huko na huko (tunaweza hata kutafsiri hili kama upanga ukatao kuwili). Siamini kwamba makerubi hawa ni viumbe wa kufikiria tu, kama kamusi fulani za kibiblia zinafafanua neno. Kwa kweli ni viumbe halisi ambao Mwenye-nguvu Yahweh aliumba kwa kusudi maalum.

Aliwaumba kwa kusudi maalum kuwa watumishi Wake, jinsi tu alivyomuumba binadamu kwa kusudi maalum. Kumbuka kwamba binadamu kwa kiasili alifurahia uhusiano wa karibu sana na Yahweh mpaka tendo lao la kwanza la dhambi. Hawa alimfuata Ibilisi Shetani na kuamini kila neno alilomwambia. Basi hapo,akaasi Yahweh, akachukua (kuiba) tunda la mti wa kujua mema na kujua mabaya. Mviringo lazima urudiwe hapa, sio tu mti wa mema na mabaya, lakini mti wa kujua mema na kujua mabaya. Yahweh alimfundisha binadamu katika njia sahihi kujiongoza mwenyewe.Alimfunza Adamu kwani alipoumbwa, Adamu hakujua kuhusu maisha ya binadamu. Ni dhahiri Yahweh alimfundisha, kwa sababu inasema katika Mwanzo 2:13 "*wayesaw Elohim*," kumaanisha Elohim aliweka amri (neno *mitzwah* linamaana ya amri) juu ya binadamu. Kwa sababu hiyo, Yahweh alimfunza binadamu sheria na kanuni za kuishi.

Leo, Ukristo kihalisi umetupa amri zote za Yahweh.Unafunza kwamba wakati Messiah alikufa, Sheria ya Yahweh iliondolewa au kubatilishwa. Hawazingatii nini Yahshua Mwenyewe alisema katika Mathayo 5:17 ***"Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua...."*** Neno kutangua hapa katika Kigiriki ni *Luo*. Moja ya fafanuzi za neno hili la Kigiriki ni*kubatilisha*. Wakati watumishi wa Kikristo kawaida wanasisitiza kwamba sheria ya kimaandiko imebatilishwa, wanafunza mafundisho ya uwongo***"Msidhani ya kuwa nilikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amini nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie."*** (Mathayo 5:17-18).

Sheria ya Yahweh haikubatilishwa wakati Messiah alikufa. Yahshua hakuja kutangua Sheria, alikuja kuikuza na kuifanya ya kuheshimika (Isaya 42:21), na kujitoa Mwenyewe kama sadaka ya patanisho kwa dhambi. Alipokuwa humu duniani, alifunza kuwa watu wake lazima watunze sheria za kiroho (Sheria za Yahweh), kama tunatumai kubarikiwa. Dhambi ni uasi, ukiukaji wa, au uvunjaji wa Sheria za Yahweh (1 Yohana 3:4). Soma ufafanuzi huu wa dhambi kwako mwenyewe. ***"Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi."***

Katika kuzingatia zaidi kwa neno *makerubi*, basi tugeuke kwa kitabu cha Ezekieli. Katika Ezekieli 1:4, tunasoma maelezo wazi ya Makerubi hawa: ***"Nikaona na tazama, upepo wa dhoruba ulitoka upande wa kaskazini, wingu kubwa sana, pamoja na moto, ukifanya duara ya nuru, na mwangaza pande zote, na katikati yake kitu kama rangi ya kaharabu, katikati ya moto huo. Kukatokea katikati yake mfano wa viumbe hai vinne. Kuonekana kwao kulikuwa hivi; walikuwa na sura ya mwanadamu. Na kila mmoja alikuwa na nyuso nne... ."***(Ezekieli 1:4-6a). Wanathiolojia wanajaribu kusisitiza kwamba wasomaji wa Biblia hawawezi kutegemea kwa uzito kwa maelezo haya, kwamba hili ni tamathali ya usemi tu, *anthropomorphism*, kitu fulani kinachoonekana katika umbo, kama mtu. Walakini sisomi hilo. Nachukua Biblia kihalisi. Kama iwezekanavyo.Yahweh hajaribu kutuchanganya katika Neno Lake, lakini kutufundisha. Utafsiri mwingine wowote ni fundisho la uwongo- fundisho hatari la uongo ambalo litawachanganya watu, kuwaelekeza kupotea. Lazima tutafsiri Biblia kihalisi kadri tuwezavyo.

Mwandishi angependa kuwakumbusha wasomaji kwamba kunao wasomi wengi wa kihafidhina wa Biblia (miongoni mwao Dr. Bernard Ramm, kwa mfano), ambao watakuelekeza kusoma Biblia kihalisi iwezekanavyo. Kunazo lugha za kitamathali kadhaa zinazopatikana katika Biblia, lakini hapa inaonekana maelezo halisi ya maono ambayo Ezekieli aliona ya Mwenye-nguvu na kiti Chake cha enzi cha mbinguni.

Jambo la kwanza ambalo Ezekieli anaona likija kutoka kwa mtikisiko huu wa moto ni viumbe vinne vilivyo hai ambavyo vinao mwonekano, au mfano wa mtu. Kuendelea kusoma katika mstari wa 6, ***"Na kila mmoja alikuwa na nyuso nne, na kila mmoja alikuwa na mabawa manne. Na miguu yao ilikuwa miguu iliyonyooka; na nyayo za miguu yao zilikuwa kama nyayo za miguu ya ndama; zikimetameta kama rangi ya shaba iliyosuguliwa sana. Nao walikuwa na mikono ya mwanadamu chini ya mabawa yao, pande zote nne, na wote wanne walikuwa na nyuso zao na mabawa yao hivi; mabawa yao yaliungana hili na hili; nao hawakugeuka walipokwenda, kila mmoja kuelekea mbele. Kwa habari za mfano wa nyuso zao, walikuwa na uso wa mwanadamu; na hao wanne walikuwa na uso wa simba upande wa kuume, na hao wanne walikuwa na uso wa ng'ombe upande wa kushoto, na hao wanne walikuwa na uso wa tai pia."*** (Ezekieli 1:6-10). Maelezo haya yanaonyesha kwamba wangeangalia kila upande wa njia na wanalo umbo la binadamu na mabawa wanayofunika mikono yao.

Kuendelea katika mstari wa 11, tunasoma, ***"Na nyuso zao na mabawa yalikuwa yametengana kwa juu; mabawa mawili ya kila mmoja yaliungana,*** [walishikana mikono]***hili kwa hili, na mawili yalifunika miili yao."***Mbele na nyuma kulikuwa na mabawa mawili na mikono chini yake, ambayo (ingeweza kuonekana) waliitumia kwa staha. ***"Nao walikwenda kueleeka mbele, kila mmoja wao; roho ilikotaka kwenda, ndiko walikokwenda, hawakugeuka walikokwenda. Kwa habari za kuonekana kwao vile viumbe hai; kuonekana kwao kulikuwa kama***



***makaa ya moto yawakayo, kama kuonekana kwa vinga vya moto; moto ule ulikuwa ukienda juu na kushuka chini, katikati ya vile viumbe hai; na ule moto ulikuwa na mwangaza mwingi, na katika ule moto ulitoka umeme."*** (Ezekieli 1:12-14).Mwendo wao ulikuwa wenye kasi mno!

Baadaye, inaelezewa gurudumu ndani ya gurudumu, kitu fulani kama *gyroscope*, ambayo pia iliambatana na maono hayo. Walakini, hatutajadili somo hilo hapa.

Katika mstari wa 22, tunaendelea, ***"Tena juu ya vichwa vya viumbe hai palikuwa na kitu mfano wa anga, kama rangi ya bilauri, lenye kutisha***[kitu kinachotoa kinzani ya nuru, ikifanya athari ya upinde wa mvua wa nuru]***limetandwa juu ya vichwa vyao. Na chini ya anga mabawa yao yamenyooshwa***[yanashikilia anga hili], ***moja kuielekea la pili; kila mmoja alikuwa na mawili yaliyowafunika miili yao upande mmoja, na kila mmoja alikuwa na mawili yaliyowafunika miili yao upande wa pili. Nao walipokwenda nilisikia mshindo wa mabawa yao, kama mshindo wa maji makuu, kama sauti ya Mwenye-enzi, mshindo wa mvumo, kama mshindo wa jeshi, hapo waliposimama walishusha mabawa yao. Tena palikuwa na sauti ya juu ya anga lile, lilipokuwa juu ya vichwa vyao; hapo waliposimama walishusha mabawa yao."*** (Ezekieli 1:22-25). Sauti iliyokuwa juu ya anga iliwaelekeza kuhusiana na mwelekeo upi wachukue na wafanye nini. Waliposikia, walijibu mara moja na kutekeleza agizo la sauti.

***"Na juu ya anga, lililokuwa juu ya vichwa vyao, palikuwa na mfano wa kiti cha enzi, kuonekana kwake kama yakuti samawi; na juu ya mfano huo wa kiti cha enzi, ulikuwako mfano kama kuonekana kwa mfano wa mwanadamu juu yake."*** (Ezekieli 1:26). Hapa ni maelezo ya maono yanayoonyesha Mwenye-nguvu Elohim. Mwenye-nguvu kwa kweli anao mwonekano wa mtu, lakini hajaumbwa na nyama na damu. Ameumbwa kwa roho. Hili ni sawa na Makerubi, kiumbe hai aliyeumbwa kwa roho.

***"Nikaona kama kwamba ni rangi ya kaharabu, kama kuonekana kwa moto ndani yake pande zote, tangu kuonekana kwa viuno vyake na juu; na tangu kuonekana kwa viuno vyake na chini, niliona kama kwamba ni kuonekana kwa moto; tena palikuwa na mwangaza pande zake zote. Kama kuonekana kwa upinde wa mvua, ulio katika mawingu siku ya mvua, ndivyo kulivyokuwa kuonekana kwa mwangaza ule pande zote...."*** (Ezekieli 1:27-28a). Inayoelezewa hapa ni kioo cha kutisha ambacho kingebadilisha nuru, ikiipa mwonekano wa upinde wa mvua. Mawingu chini ya Mwenye-nguvu yana mwonekano wa yakuti (rangi ya bluu ya kina). Tunaona basi kwamba, ***"Ndivyo kulivyokuwa kuonekana kwake mfano huo wa utukufu*** (*kavod* katika Kiebrania) ***wa Yahweh. Nami nilipoona nilianguka kifudifudi, nikasikia sauti ya mmoja anenaye."*** (Ezekieli 1:28b). Maono ambayo Ezekieli anaelezea ni yenye nguvu na yanaonyesha kwetu nguvu ya kushangaza na kuu ya Yahweh na ya viumbe Vyake vilivyoumbwa, Makerubi.

Hapa sio tu mahali ambapo tunakutana na maelezo ya makerubi. Makerubi pia wanaelezewa katika Ezekieli 10.***"Ndipo nikaangalia, na tazama, katika anga lililokuwa juu ya vichwa vya makerubi, kulionekana kama mfano wa kiti cha enzi."*** Hapa ni maelezo ya mwanga unaotoka kutoka kwa kiumbe huyu mkuu wa kiroho na kutoka kwa kiti Chake cha Enzi kilicho juu ya jukwaa hili. Ezekieli 10:4 inaendelea, ***"Utukufu wa Yahweh ukapaa kutoka kwa kerubi yule,ukasimama juu ya kizingiti cha nyumba, nayo nyumba ikajazwa na lile wingu, na ua ulikuwa umejaa mwangaza wa utukufu wa Yahweh."*** Wingu hili la utukufu kwa kawaida linapewa istilahi utukufu wa *shekinah*. Neno utukufu wa *shekinah* ni kutoka kwa neno *shekan* ambalo katika Kiebrania lina maana ya kukaa. Walakini, neno *shekinah* hata halijatumiwa katika Biblia katika maana hii ya kuihusisha kwa Mwenye-nguvu. Kwa sababu hiyo, hapa inaonekana maelezo ya Mwenye-nguvu na maelezo ya msafara Wake, usafiri Wake, na Ulinzi Wake.

Tumeanzisha maelezo ya darasa la kwanza la viumbe walioumbwa (makerubi) ambao moja kwa moja wanamtumikia Mwenye-nguvu Yahweh. Tutaendelea kuendeleza somo hili katika siku zijazo, kama tunabaini maelezo zaidi ya Yahweh na viumbe wake walioumbwa. Maana yake itaonyesha kwamba moja kwa moja wanaathiri wokovu wa binadamu.

Hili kwa kweli ni somo la ajabu. Tunatumai kwamba kamwe hautakosa kuunga nasi kwa programu za **Sacred Name**, ama kwa redio au televisheni, na kwamba utatuandika kwa nakala za bure juu ya hili na mada zingine mingi muhimu za kibiblia. Andika kwa Assemblies of Yahweh, Po Box, Bethel, Pennsylvania 19507. Ungana na huduma hii, kwa sababu bila shaka utanufaika sana kutokana na mambo utakayojifunza. SNB

# Viumbe vya Yahweh Vilivyoumbwa

### Sehemu ya 2

Maandiko Matakatifu yanajumuisha *magnum opus* ya maandishi yote. Ni kazi ya fasihi kuu zaidi ambayo iliwahi kutolewa, kwa sababu iliandikwa na akili inayoishi katika umilele. Aliwaongoza waandishi wa Biblia kuandika anachotaka binadamu kujua na kuelewa kuhusu maisha. Magnum opus hii inapaswa kuwa kitabu cha msingi cha maagizo kwa maisha yetu. Umaarufu wake kupitia kwa karne umekuwa usiyo na kifani.

Maandiko Matakatifu sio tu kitabu cha msukumo, ingawa watu wengi wa dini katika nyakati za shida wanazingatia juu ya Zaburi. Kitabu cha Zaburi kinatoa msukumo mkubwa katika nyakati hizi za majaribu. Nilipokuwa kijana mdogo, familia yangu ilihamasisha kusoma kwa Zaburi 91 kama mjenzi-mkuu-wa-imani. Nakumbuka nilipokuwa kijana, kama mtu angejeruhiwa, na kutokwa na damu hakukusimama haraka, wangesema, "Sasa ni wakati wa kuwa na imani. Tutasoma Zaburi 91." Kawaida, kwa wakati tunafikia mwisho wa Zaburi kuvunja damu kulikuwa kumesimama, Mwenye-nguvu Yahweh alikuwa amefanya miujiza na kwa shukrani hivyo.

Ni katika mifano kama hii na kupitia utafiti wa makini ambapo nimekuwa muumini mkubwa katika Biblia. Naipenda! Naifunza hapa katika Obadiah School of the Bible. Hakuna kitabu kingine kabisa kama hicho. Cha kusikitisha, ujumbe wake kamili umeweza kutoeleweka, kunukuliwa vibaya, kutumika vibaya na hata kukataliwa na baadhi kwa karne mingi. Sasa katika siku hizi za mwisho, kama maarifa yanaongezeka, nashangaa kwa mambo Yahweh anafunua, hata baada ya zaidi ya miaka 40 ya utafiti wa makini wa Biblia. Mbinu kwa kuelewa vizuri ujumbe wa kimaandiko ni kuoanisha Biblia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo na kuiruhusu ijisemee yenyewe.

Nimekuwa nikijadili somo la madarasa manne ya viumbe vilivyoumbwa ambao Mwenye-nguvu Yahweh aliumba, kuwa wenzake na watumishi Wake. Katika programu ya mwisho, somo la majadiliano lilikuwa binadamu. Kabila ya Adamu ni binadamu. Katika Zaburi 8, swali linaulizwa, "***Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na binadamu hata umwangalie? Umemfanya mdogo punde kuliko Elohim***[**King James Version** inatafsiri neno hili malaika, lakini Biblia ya Kiebrania inalo Elohim]…"

Elohim linajumuisha darasa la viumbe wanaoishi milele ambao jina lao ni Yahweh. Familia hii ya Elohim inajumuisha Yahweh aliye Baba na Yahshua aliye Mwana, katika Agano la Kale. Tafadhali gundua Zaburi 68:4. Yahshua aliye Mwana alijulikana kama Neno la Yahweh- Msemaji wa Yahweh- mwakilishi Wake kwa binadamu. Yahweh aliumba binadamu kutunza, na kuweka katika hali nzuri, bustani la Edeni alilopanda duniani. Baadaye, Yahweh aliweka juu ya mabega ya binadamu jukumu la kutunza dunia nzima.Alikuwa amemweka mtu katika bustani nzuri (Bustani la Edeni lililoitwa *Gan Eden*katika Kiebrania).

Shamba hili nzuri liliteuliwa kama nyumbani kwa binadamu, mpaka binadamu walipofanya dhambi, na kula mti wa kujua mema na kujua mabaya. Adamu akabeba hatia yake, kwa sababu Mwenye-nguvu Yahweh alimwagiza yeye katika Mwanzo 2:16, akisema, "waysaw Yahweh Elohim alha'adam," au ikitafsiriwa:**"Na Yahweh Elohim akamwekea amri huyo mtu…."**

Yahweh alimwambia Adamu: "Utafanya," au "Usifanye," vitu fulani. Wakati binadamu anakataa mamlaka ya Yahweh kupitia kutotii na kufuata maagizo ya shetani Ibilisi kufanya kama anavyopenda, basi, Yahweh ilibidi atende. Matokeo ya dhambi ya binadamu ilikuwa kwamba alifukuzwa nje ya Bustani tukufu la Edeni. Juu yake, Yahweh akaweka kwa kiingilio cha bustani walinzi wanaoitwa *makerubi*. Walinzi hawa walidumisha upanga wa moto unaogeuka "huko na huko" kumzuia mtu asirudi shamba la Edeni. Mtu hawezi kurudi shamba la Edeni kwa sababu ya dhambi zake. Tunatamani kurejeshwa kwa Bustani la Edeni katika wakati Ufalme wa Yahweh unatawala dunia hii. Kisha itaanzishwa anga ya amani na utulivu utakaofunika sayari hii yote. Ninasoma Biblia,



kwa sababu ninatamani kuwa hapo, na ninajua kuwa unao mwelekeo sawa.

Tulijadili kwa kifupi neno *makerubi* katika awamu iliyopita ya msururu huu. Tulichambua maelezo yanayoonekana katika Ezekieli 1, na kisha, tukageuka kwa Ezekieli 10, ambapo somo linashughulikiwa. Mwisho wa sura hii unasema, ***"Nikajua kwamba walikuwa makerubi."*** Neno *makerubi* katika Kiebrania linatamkwa kwa sauti ya awali ya k-, sio kama inavyowakilishwa kawaida katika Kiingereza kwa sauti ch-. Lazima tukumbuke matamshi haya ya kibiblia sahihi zaidi yanayoonekana katika nakala ya Kiebrania, hata ingawa tutaendelea na maendelezo ya desturi ya Kiingereza.

Katika sehemu hii, tutazingatia kifungu cha Kutoka 25. Yaliyo kwenye kifungu hiki yanaonekana maelezo ya Musa akijenga hema ya Israeli nyikani, na pia akipewa muundo kwa fanicha zote za hema, baadhi ya ambazo ziliingizwa kwenye Hekalu ya Suleimani.

***"Nao na wafanye sanduku la mti wa mshita; urefu wake na uwe dhiraa mbili na nusu, na upana wake dhiraa moja na nusu, na kwenda juu kwake dhiraa moja na nusu. Nawe ulifunike kwa dhahabu safi, ulifunike ndani na nje, nawe tia na ukingo wa dhahabu kulizunguka pande zote. Nawe subu vikuku vinne vya dhahabu kwa ajili yake, na kuvitia katika miguu yake minne; vikuku viwili upande mmoja, na vikuku viwili upande wake wa pili. Nawe fanya miti mirefu ya mshita na kuifunika dhahabu. Nawe tia hiyo miti katika vile vikuku vilivyo katika pande mbili za sanduku ili kulichukua hilo sanduku. Hiyo miti itakaa katika vile vikuku vya sanduku; haitaondolewa. Kisha tia ndani ya sanduku huo ushuhuda nitakaokupa***[hizo ni mbao mbili za mawe]***. Nawe fanya kiti cha rehema cha dhahabu safi***[Neno ni *cappareth* katika Kiebrania, *kifuniko* au *kiti cha rehema cha dhahabu safi*. Ni kifuniko kitakachotoshea juu ya sanduku]***; urefu wake utakuwa dhiraa mbili na nusu, na upana wake dhiraa moja na nusu."***(Kutoka 25:10-17).

Inayoelezewa hapa ni sanduku la mbao, urefu wa dhiraa moja na nusu, upana wa dhiraa moja na nusu, na kwenda juu dhiraa moja na nusu. Inchi ishirini na mbili ni urefu unaokubalika kawaida wa dhiraa wa kibiblia, hivyo sanduku hili lingekuwa kitu kati ya karibu fiti tano urefu na takribani, futi

mbili na robo tatu upana na kwenda juu. Inayoelezewa hapa kwa kweli ni masanduku matatu. Sanduku la mbao lililofunikwa nje na ndani kwa dhahabu. Maelezo haya yanaonyesha hazina iliyolindwa sana kwa Amri Kumi, mbao za mawe ambazo amri za Yahweh ziliandikwa.

Kama tutaendelea kusoma hapa katika Kutoka 25, tutakutana na neno *makerubi* katika mstari wa 18. ***"Nawe fanya makerubi mawili ya dhahabu; uyafanye ya kazi ya kufua, katika hiyo miisho ya kiti cha rehema, huku na huku. Weka kerubi moja mwisho mmoja, na kerubi la pili mwisho wa pili, fanya hayo makerubi ya kitu kimoja na kiti cha rehema***[pamoja na *cappareth*, kifuniko]***, mwisho huku na mwisho huku. Na hayo makerubi yatainua mabawa yao juu, na kukifunika hicho kiti cha rehema, kwa mabawa yao, na nyuso zao zitaelekeana hili na hili; nyuso za hayo makerubi zitaelekea kiti cha rehema. Weka kiti cha rehema juu ya sanduku, kisha utie huo ushuhuda nitakaokupa ndani ya sanduku. Nami nitaonana nawe hapo...."***

Kifungu hiki kinaelezea nakala ya kiti cha enzi cha Yahweh. Yahweh huketi katikati ya *makerubi*(Zaburi 99:1) juu ya kiti cha enzi cha sanduku Lake ambalo ushuhuda ulio karibu na yeye, au makubaliano ya Agano lililofanywa kati ya Yahweh na binadamu. ***"Na kuzungumza nawe pale nilipo juu ya kiti cha rehema, katikati ya hayo makerubi mawili yaliyo juu ya sanduku la ushuhuda, katika mambo yote nitakayokuagiza kwa ajili ya wana wa Israeli."***

Inayoelezewa hapa ni makerubi mmoja akipiga magoti upande mmoja wa kifuniko cha sanduku huku mabawa mawili yaliyonyoonshwa kuelekea kwa makerubi mwingine anayepiga magoti mwisho mwingine wa *cappareth*(kifuniko) akiwa na mabawa yake yamenyooshwa. Ulioonekana katikati ya makerubi ulikuwa utukufu wa Yahweh. Picha yenye kushangaza vipi tuliyopewa hapa!

Basi turudi nyuma tena na kusoma maelezo mafupi yanayopatikana katika Ezekieli 10:20. ***"Huyu ndiye kiumbe hai niliyemwona, chini ya Elohim wa Israeli, karibu na Mto Kebari, nikajua ya kuwa hao ni makerubi. Kila mmoja alikuwa na nyuso nne, na kila mmoja alikuwa na mabawa manne, na mifano ya mikono ya mwanadamu ilikuwa chini ya mabawa yao. Na mfano wa nyuso zao, ni nyuso zile zile nilizoziona karibu na Mto Kebari; kuonekana kwao, na wao wenyewe; kila mmoja walikwenda mbele moja kwa moja."***

Kama tutageuka tena kwa mlango wa kwanza wa Ezekieli, maelezo ya viumbe hawa hai wanne inaonekana. ***"Kuonekana kwao kulikuwa hivi; walikuwa na sura ya mwanadamu. Na kila mmoja alikuwa na nyuso nne, na kila mmoja alikuwa na mabawa manne. Na miguu yao ilikuwa miguu iliyonyooka, na nyayo za miguu yao zilikuwa kama nyayo za miguu ya ndama; zikimetameta kama rangi ya shaba iliyosuguliwa sana.[***waling'aa kwa rangi***] Nao walikuwa na mikono ya mwanadamu chini ya mabawa yao, pande zote nne, na wote wanne walikuwa na nyuso zao na mabawa yao hivi; mabawa yao yaliungana hili na hili; nao hawakugeuka walipokwenda kila mmoja kuelekea mbele. Kwa habari za mfano wa nyuso zao, walikuwa na uso wa mwanadamu; na hao wanne walikuwa na uso wa simba upande wa kuume, na hao wanne walikuwa na uso wa ng'ombe upande wa kushoto, na hao wanne walikuwa na uso wa tai***[ingeashiria kwamba ilikuwa nyuma ya vichwa vyao]. ***Na nyuso zao na mabawa yalikuwa yametengana kwa juu; mabawa mawili ya kila mmoja yaliungana, hili kwa hili, na mawili yalifunika miili yao "*** (Ezekieli 1:5b-11). Inayoonekana hapa ni maelezo wazi ya makerubi wanaofunika, wanaoonyeshwa katika uwakilishaji wao juu ya sanduku la hema.

Basi tugeuke kwa Ezekieli 28. Mlango huu unaelekezwa kwa mfalme wa Tiro. Kumbuka kwamba Tiro ulikuwa mji wa Foineke (mji wa Waakanani) pwani za Mediterenea katika inajulikana sasa Lebanoni, kaskazini mwa Israeli. Lazima tuulize, "kwa nini kifungu hiki kimeelekezwa kwa Mfalme wa Tiro?" Jibu ni kwa sababu Wafoinike (Wakanani) walikuwa waabudu wa Baali. Hawakuwa waabudu wa Yahweh. Lililo kwenye eneo la kaskazini mwa Israeli, tunapata eneo la Ras Shamra (Ugarit), ambalo lilikuwa kituo cha ibada ya kale ya Baali.Maktaba katika Ras Shamra, iliyogunduliwa takribani miaka 100 iliyopita, inaonyesha kwamba eneo hili linajumuisha kituo cha ibada hii ya upagani. Inaonekana kwamba kifungu hiki kinaelekezwa dhidi ya taifa linaloabudu Baali, na mfalme wa taifa hilo (taifa la Wafoinike, au Lebanoni kwa wakati huo) aliitwa Ethbaali. Jezebeli alikuwa binti ya mfalme Ethbaali, 1 Wafalme 16:31. Hiram alikuwa dhahiri mtangulizi wa mfalme huyu wa kanani Ethbaali. Jina Ethbaal linaweza kutafsiriwa kama *kihusishi cha Kisemitiki eth (pamoja na),na Baali* (*uabudu wa ma-bwana wa*



***"Ulikuwa ndani ya Edeni, bustani ya Elohim; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako, akiki, na yakuti manjano, na almasi, na zabarajadi, na shohamu, na yaspi, na yakuti samawi, na zumaridi, na baharamani, na dhahabu...."***

EZEKIELI 28:13A

Tunapata hapa kuorodheshwa kwa mawe tisa, mawe sawa na yale yanayoonekana katika dirii ya kifuani ya hukumu ya kuhani Mkuu wa Yahweh; walakini, tatu ya mawe yaliachwa

Ni wazi kwamba Shetani alikuwa na fursa ya kufikia kwa kidogo kabisa ya maarifa, lakini sio kwa maarifa yote ya mpango wa wokovu ambao Yahweh aliyatoa juu ya watu Wake Israeli. Zingatia pia kwamba nambari 9 inaashiria mwisho wa hukumu, wakati nambari 12 (idadi ya mawe katika kifuniko cha kifuani cha kuhani mkuu) iliashiria serikali nzuri.

*eneo)*, hilo ni, pamoja na Baali. Ni wazi mfalme wa Tiro alikuwa mwabudu wa Baali. Pia alikuwa kuhani wa Baali katika iliyokuwa Foinike. Kama matokeo, unabii huu haujaelekezwa tu kwa kuhani mkuu wa Baali, lakini pia, kuelekea nguvu nyuma ya kiti cha enzi, Shetani, adui ya mwenye-nguvu Yahweh.

Ni nani nguvu ya ibadi ya uasi duniani leo? Geuka kwa Ezekieli 28:11-13a, **"Tena neno la Yahweh likanijia, kusema, Mwanadamu, umfanyie maombolezo Mfalme wa Tiro, umwambie, Mwenye-enzi Yahweh asema hivi; wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima, na ukamilifu wa uzuri. Ulikuwa ndani ya Edeni, bustani ya Elohim**[mfalme wa Tiro kamwe hakuwa katika Edeni, bustani la Elohim**] kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako..."**

Tunapata hapa kuorodhesha kwa mawe tisa, mawe sawa na yale yanayoonekana katika kifuniko cha kifuani cha hukumu cha kuhani Mkuu wa Yahweh; walakini, tatu ya mawe yaliachwa.


Linganisha Kutoka 28:17-20 na Ezekieli 28:13. Ni wazi kwamba Shetani alikuwa na fursa ya kufikia kwa kidogo kabisa ya maarifa, lakini sio kwa maarifa yote ya mpango wa wokovu ambayo Yahweh aliyatoa juu ya watu Wake Israeli. Zingatia pia kwamba nambari 9 inaashiria mwisho wa hukumu, wakati nambari 12 (idadi ya mawe katika kifuniko cha kifuani cha kuhani) kiliashiria serikali nzuri.

Ezekieli 28:13 kisha inaendelea, ***"Katika siku ya kuumbwa kwako zilitengenezwa tayari. Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye...."*** Neno kutiwa mafuta hapa-*mimshach* katika maandishi ya Kiebrania- ni sawa kama mzizi wa neno *Meshiach* au *Messiah*. Tafadhali angalia **Hebrew Dictionary of Strong's Exhaustive Concordance**, nambari 4473, 4886, na 4899. Sasa soma ukiwa na maarifa hayo akilini, ***"Wewe ulikuwa kerubi wa Messiah afunikaye; nami nilikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Elohim, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto.Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako. Kwa wingi wa uchuuzi wako watu walikujaza udhalimu ndani yako...,"*** na anaendelea kusema,***"Nami nimekuangamiza, Ewe kerubi afunikaye***[neno *cassah* limetumika hapa, limetolewa kufunika], ***utoke katika mawe hayo ya moto."***

Anayeelezewa hapa kama makerubi mmoja angekuwa Adui aliye Shetani. Shetani Ibilisi ni nguvu nyuma ya kiti cha enzi cha mafundisho yote ya uwongo na dini potofu kwenye uso wa dunia. Daima anajaribu kuwageuza watu mbali na mpango wa Yahweh wa wokovu. Kumbuka, kulikuwa na makerubi wawili walioonyeshwa juu ya kifuniko cha sanduku. Mmoja alikuwa makerubi aliyepakwa mafuta afunikaye, ambaye alimkataa Yahweh na kuwa ibilisi Shetani, Adui kwa Mwenye-nguvu Yahweh. Ni nani tuseme alikuwa huyo mwingine? Huyo ni kiumbe mwaminifu aliyeumbwa, aliyekuwa Messiah(Meshiach), Mwokozi wetu, Yahshua aliye Messiah. Anaelezewa katika Zaburi 2:2 kama mtiwa mafuta wa Yahweh, Messiah Wake. Alikuwa Mwana mwaminifu ambaye, kupitia haki yake, atapokea utawala wa Ufalme wa Yahweh. **"Nami nimemweka mfalme wangu juu ya Sayuni, mlima wangu mtakatifu. Nitaihubiri amri; Yahweh aliniambia, ndiwe mwanangu, mimi leo nimekuzaa. Uniombe, nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako, na miisho ya dunia kuwa milki yako. utawaponda kwa fimbo ya chuma, na kuwavunja kama chombo cha mfinyanzi."** (Zaburi 2:6-9).

Tutaendelea na utafiti huu kama tunazingatia zaidi darasa zote za viumbe wanne walioumbwa wa Yahweh. Kama Neno la Yahweh linakuwa wazi kwenye mbao, tunaweza waziwazi kutambua maoni kubwa ya mpango kamili wa Yahweh kwa watu Wake na jinsi tunaingia ndani yake.

Kama tunajifunza zaidi ya mada hizi za kina za kibiblia, tunakua katika neema za maarifa na kuwa watumishi Wake watiifu. Kwa nini usiwasiliane na huduma hii leo na kujifunza zaidi ya kweli hizi za kina za kibiblia? Andika kwa: Assemblies of Yahweh, PO. Box C, Bethel, Pennsylvania 19507, kwa nyenzo zetu ziada za kusoma. SNB



# THE LAW OF YAHWEH

## Amri ya Tisa

# Usimshuhudie Jirani yako Uongo

Na Mzee Jacob O. Meyer

*“Lakini mtu mmoja jina lake Anania pamoja na bibiye Safira, aliuza mali, akauza kwa siri sehemu ya thamani yake, mkewe naye akijua haya, akaleta fungu moja akaliweka miguuni pa mitume. Petro akasema, Anania, kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu, na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja? Kilipokuwa kwako, hakikuwa mali yako? Na kilipokuwa kimekwisha kuuzwa, thamani yake haikuwa katika uwezo wako?Ilikuwaje hata ukaweka neno hili moyoni mwako? Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Yahweh. Anania aliposikia maneno haya, akaanguka akafa.Hofu nyingi ikawapata watu wote waliosikia maneno haya.Vijana wakaondoka, wakamtia katika sanda, wakamchukua nje, wakamzika.*

*“Hata muda wa saa tatu baadaye mkewe akaingia, naye hana habari ya hayo yaliyotokea. Petro akamjibu, Niambie, mlikiuza kiwanja*

***kwa thamani hiyo? Akasema, Ndiyo, kwa thamani hiyo. Petro akamwambia, Imekuwaje hata mkapatana kumjaribu Roho wa Yahweh? Angalia, miguu yao waliomzika mumeo ipo mlangoni, nao watakuchukua nje na wewe nawe. Mara akaanguka miguuni pake akafa; wale vijana wakaingia wakamkuta amekufa, wakamchukua nje, wakamzika pamoja na mumewe. Hofu nyingi ikawapata Kusanyiko lote na watu wote walioyasikia haya."***(Matendo ya Mitume 5:1-11).

Somo la kimandiko mbele yetu leo ni amri ya tisa, inayopatikana katika Kutoka 20:16 na kurudiwa katika Kumbukumbu la Torati 5:20 (miongoni mwa mahali kwingine). "***Usimshuhudie jirani yako uongo."*** Lazima tubainishe kwamba katika maandishi ya Kiebrania neno *jirani* linakuja kutoka kwa neno la Kiebrania rea' [ray'-ah] (#7453 katika **Strong's Exhaustive Concordance of the Bible Hebrew Dictionary**), kumaanisha *mshirika* (*karibu zaidi au kidogo), pia kaka, mwenzi, rafiki, jirani.*

Watu wengi wamefafanua amri hii kumaanisha pekee kwamba mtu hapaswi kusambaza maoni kuhusu jirani yake ambayo si kweli, au haswa zaidi, kwamba mtu hapaswi kusema uongo kwenye kizimba cha mashahidi katika kesi kortini. Daima kuambia ukweli, kweli ni utafsiri wa msingi wa amri. Walakini, kwani Yahshua aliye Messiah, Mwokozi wetu alikuja kukuza Sheria ya Yahweh na kuifanya ya kuheshimika zaidi, au inayostahili heshima (Isaya 42:21), amri hii inapaswa kutafsiriwa katika umri huu mpya wa kusambazwa kwa neema kama,kutopanua ukweli kwa njia yoyote, umbo au sura kwa kuongezea, kutoambia uongo kwa aina yoyote.

Sikia nini Sheria inaweka katika Maandishi ya Agano la Kale, katika Walawi 19:11, ***"Msiibe, wala msidanganye, wala msiambiane uongo."*** Kusema aina yoyote ya uongo, kuongezea ukweli, kusema uongo mmoja kwa mwingine, hata kuwa mdanganyifu au makusudi kupotosha watu, kamwe haijaidhinishwa na Mwenye-nguvu Yahweh.

Tunasoma katika Yohana 17:17, ***"Uwatakase kwa ile kweli, neno lako ndilo kweli."*** Tunajua kutoka kwa amri hii kwamba kupotoka kwa aina yoyote kutoka kwa dhana hii wazi ya haki ni kutoka kwa adui, Shetani Ibilisi. ***"Atendaye dhambi ni wa Ibilisi,kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Elohim alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi."*** (1 Yohana 3:8).

Tumeona hivi karibuni kwamba viongozi wanaojulikana sana, maarufu wa kidini wamewaambia wasikilizaji wao, kwamba chochote kinakubalika kikamilifu ikiwa kinahudumu kusudi sahihi. Hata ngono haramu, kuishi katika dhambi na ushoga, *euthanasia*(inayojulikana "mauaji ya huruma"), kuiba, na uongo, hazilaaniwi na watumishi wengi, ilimradi tu mtu anaamini kwamba kusudi linahudumiwa. Nani ambaye anawezafanya maamuzi kama hayo kwa njia sahihi? Binadamu? Bila shaka la! Mwenye-nguvu Yahweh katika Neno lake hajaruhusu kupotoka kutoka kwa ukweli, sio hata inayojulikana "uongo mweupe".

Walakini, watu wa kidunia hawaonekani kugundua kwamba kuna kiwango kimoja kizima, kisicho na upendeleo ambacho Mwenyenguvu Yahweh ameanzisha katika Maandiko Matakatifu kudhibiti maisha yetu ya maadili. Kiwango hicho ni Sheria ya Kifalme ya uhuru na upendo kiini ambacho ni amri 10. Binadamu kamwe hawawezijua jinsi ya kujitawala wenyewe, jinsi ya kufanikisha maisha ya furaha yenye matunda, bila kufuata na kutekeleza kanuni za maisha ya haki, Sheria za maisha zilizowekwa kwetu katika kitabu cha sheria cha Yahweh kwa maisha ya furaha- Maandiko yaliyoongozwa. Lazima tukumbuke kwamba Sheria ya Yahweh ya uhuru inatuokoa kutoka kwa sheria ya dhambi na kifo, ili kwamba tunaweza kupokea maisha ya milele katika zama za Ufalme Wake unaokuja.

Kusema isiyo kweli (kusema uongo ukipenda) imepigwa marufuku na amri za Yahweh kama moja ya dhambi ambazo kweli zitaleta uharibifu ikiwa mtu hatatubu na kugeuka kutoka kwake. Tambua jinsi Mwenyenguvu Yahweh, katika Mithali 6:16-19, tayari amehukumu uwongo kuwa chukizo. ***"Kuna vitu sita anavyovichukia Yahweh; naam, viko saba vilivyo chukizo kwake. Macho ya kiburi, ULIMI WA UONGO, na mikono imwagayo damu isiyo na hatia; Moyo uwazao mawazo mabaya; Miguu iliyo myepesi kukimbilia maovu; SHAHIDI WA UONGO ASEMAYE UONGO; naye APANDAYE MBEGU ZA FITINA KATI YA NDUGU."***

Tano ya sifa hizi saba ambazo Yahweh anachukia ZINAHUSIANA MOJA KWA MOJA KWA UONGO. Macho ya kiburi inaweza kufafanuliwa kama kujidanganya mwenyewe, kujifanya kuwa kitu usichokuwa. Ulimi wa uongo unachukiwa na Aliye Juu kwa kuwa wa kudanganya, kupotosha mtu mwingine. Yahweh anachukia moyo uwazao mawazo mabaya, kwa kujifanya kwamba mambo na hali sio jinsi inaonekana. Anachukia shahidi wa uwongo anayesema uwongo, kwani mtu




anaweza kufanya uharibifu mkubwa kwa maisha ya mtu mwingine kwa kueneza uvumi mbaya, kashfa, na kudanganya. Tumeona katika matukio mbalimbali jinsi watu walifanywa wa kuteseka shida kali kwa sababu ya shahidi wa uwongo katika kesi ya korti. Watu fulani wasio na hatia hata wamehukumiwa kifo kama matokeo ya uwongo, unaotokana kwa ushuhuda wa uwongo. Mtu fulani aliyeshtakiwa na kuachiliwa aliuliza, "sasa nani atanirudishia sifa yangu?"

Zaidi, wakati mtu anapanda mbegu ya fitina kati ya ndugu, hili linachukiwa, kwa sababu ndugu, haswa wanapaswa kupendana na kuheshimiana katika kweli- uongo utatenganisha ndugu na marafiki. (Mithali 16:27-28 na 19:5). ***"Chakula cha uongo ni kitamu kwa mtu; lakini halafu kinywa chake kitajaa changarawe."*** (Mithali 20:17). Wakati mtu anasema chochote kitakachodhoofisha hisia ya pamoja ya kuheshimiana na upendo miongoni mwa ndugu, anamfanya Yahweh mwongo, ambaye Mwenyewe ni upendo ulio-mtu.

***"Achukiaye huficha chuki kwa midomo yake; Naye huweka akiba ya hila moyoni mwake: Anenapo maneno mazuri usimsadiki; kwa maana ana machukizo saba moyoni mwake: Ingawa chuki hufunikizwa kwa hila,uovu wake utadhihirishwa mbele ya kusanyiko. Achimbaye shimo atatumbukia mwenyewe; naye abingirishaye jiwe litamrudia. Ulimi unenao uongo huwachukia wale uliowajeruhi; na kinywa cha kijipendekeza hutenda uharibifu."*** (Mithali 26:24-28).

Katika unabii wake, nabii Hosea amechora picha ya maneno ya wakati mbaya katika historia ya Israeli ambapo dhambi itakuwa imeenea. Unabii huu unaweza hudumu vizuri kama picha ya siku za kisasa ya Marekani. Basi tusome kutoka kwa mlango wa nne wa Hosea. ***"Lisikieni neno la Yahweh, enyi wana wa Israeli; kwa maana Yahweh ana mateto nao wakaao katika nchi, kwa sababu hapana kweli, wala fadhili, wala kumjua Elohim katika nchi. Hapana neno ila kuapa kwa uongo, na kuvunja ahadi, na kuua, na kuiba, na kuzini; huruka mpaka, na damu hugusana na damu."***(Hosea 4:1-2). Gundua kwamba dhambi hizi zote zinazozalisha ubishani kati ya Yahweh na uumbaji wake wa binadamu unahusiana kwa ukiukaji wa Amri 10, ukiukaji ambao Yahweh ameuhukumu wa kustahili kifo, na adhabu hii ya kifo itakuwa hatima ya mwishowe ya mkosaji. Mshahara (thawabu) wa dhambi ni kifo (Warumi 6:23).

Tambua pia mstari wa 6 wa Hosea mlango wa 4, ***"Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi; kwa kuwa umeisahau sheria ya Elohim wako, mimi nami nitawasahau watoto wako ."*** Kweli maneno haya ni yenye uzito kweli, kama Yahweh ametamka maamuzi Yake kwa Waisraeli wa siku hiyo. Kuongezea, ni dhahiri kwamba Yahweh habadiliki (Malaki 3:6); kwa hivyo, tunaweza vizuri kutumia maonyo hayo kwa wakati wetu. Hakika, ushahidi unathibitisha Neno la Yahweh ni la kutumika kupitia mawimbi yanayopanda ya uzinzi leo.

Nabii Amosi anapiga kelele kwa maneno sawa ya adhabu ambayo Yahweh amemwamuru kusema, ***"Haya ndiyo asemayo Yahweh; kwa makosa matatu ya Yuda, naam, kwa manne, sitaizuia adhabu yake isimpate, kwa sababu wameikataa sheria ya Yahweh; wala hawakuzishika amri zake; na maneno yao ya uongo yamewakosesha, ambayo baba zao waliyafuata."*** (Amosi 2:4). Hapa tena, kusema uongo imeunganishwa kwa karibu na ukiukaji wa Amri 10 za Yahweh.

Katika kifungu cha kimaandiko tulichosoma kufungua matangazo haya ya redio, tulitambua kwamba Anania na Safira, washiriki wa Kusanyiko la Kitume, waliuza ardhi fulani waliyomiliki ili kuchangia kwa kutegemeza kusanyiko la Agano Jipya la Yahweh. Ardhi nzima ilikuwa yao kufanya watakalo. Waliuza, lakini wakaweka(kuhifadhi) sehemu ya bei ya ardhi kwao wenyewe,

wakati wanaweka mitume chini ya hisia ya uongo kwamba walitoa thamani yote kwa Yahweh kwa matumizi katika kazi Yake. Dhambi haikuwa katika kuzuia sehemu ya bei iliyouzwa, lakini kwamba walisema uwongo kwa Roho Mtakatifu wa Yahweh Mwenye-nguvu.(Matendo ya Mitume 5:4-9).

Kitendo hiki kilikuwa karibu kwa kiwango sawa na busu Yuda Iskariote alimpa Mwokozi wetu katika bustani la Gethsemane alipomsaliti. Busu inaashiria upendo wa undugu, wakati kweli, busu hili la Yuda lilikuwa uongo, busu la kisasi linaloonyesha chuki na usaliti.***"Ingawa chuki hufunikizwa kwa hila;uovu wake utadhihirishwa mbele ya kusanyiko."*** (Mithali 26:26). Unakumbuka kuwa Yuda pia alikuwa mwizi (Yohana 12:4-6)? Yuda aliiba kutoka kwa hazina yake Messiah mwenyewe.

Roho Mtakatifu kupitia kwa Ufunuo uliotolewa kwa Yohana anatuambia ni nani atastahiki kuingia maisha ya milele, Ufalme wa Mbinguni, na mji wake unaotawala, Yerusalemu Mpya. ***"Heri wazishikao amri zake, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake.Huko nje wako mbwa, na wachawi, na wazinzi, na wauaji, na hao waabuduo sanamu, na kila mtu apendaye uongo na kuufanya."*** (Ufunuo 22:14-15).

Zote kupenda uongo na kufanya uongo, zinazingatiwa kuwa kwa kiwango sawa na zinatangazwa na Yahweh kuwa dhambi itakayowaweka ambao wanayafanya matendo kama hayo nje ya Ufalme wa Yahweh. ***"Maana torati yote imetimilika katika neno moja, nalo ni hili, umpende jirani yako kama nafsi yako. Lakini mkiumana na kulana, angalieni msijemkaangamizana."*** (Wagalatia 5:14-15).

Leo, sisi zote tunajitahidi kufikia nyumbani tuliyoahidiwa ya milele, Ufalme wa Yahweh, utakaotawala kwa utawala mkuu katika haki juu ya dunia hii kwa milenia. Agano ambalo limetolewa kwa binadamu ni rahisi sana-utiifu kwa Neno la baba wetu wa Mbinguni Yahweh Elohim na kukubali kwa sadaka yake ya dhabihu ya upendo ya Mwana Wake mzaliwa wa pekee kwa dhambi tulizofanya. Sasa lazima tuwe kwa tabia zetu nzuri katika kutunza amri za Yahweh kwa uaminifu, Ufunuo 12:17 na 14:12.

Waebrania 10:26-29 inafanya hili wazi zaidi. **"Maana kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto utakaowala wao wapingao. Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa neno la mashahidi wawili au watatu. Mwaonaje, haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyanga Mwana wa Elohim, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema?"**

Ni kwa nani utapiga kura yakoleo? Utachagua upande wa Yahweh Mwenye-nguvu na Yahshua aliye Messiah, Mwana Wake, Mwokozi wetu, au utachagua njia ya adui-mkuu wa Sheria na mpangilio, Ibilisi Shetani? Yeye ndiye aliyeelezea uongo wa kwanza uliorekodiwa kwenye Biblia (Mwanzo 3:4), na kwa hivyo, Shetani ni baba ya uwongo.***"Ninyi niwa baba yenu Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa sababu hakuna ukweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo."*** Anasema Messiah mwenyewe katika Yohana 8:44. Kumbuka, katika vita iliyo bado ya Harmagedoni, Mwenye-nguvu Yahweh atakuwa mshindi; bakia upande Wake!

Ninakuacha leo na wazo hili, linalopatikana katika Tito 1:2 ***"Katika tumaini la uzima wa milele, ambalo Yahweh asiyeweza kusema uongo aliuahidi tangu milele."*** Mwandishi wa Waebrania anathibitisha wazo hili. ***"Maana wanadamu huapa kwa yeye aliye mkuu kuliko wao; na kwao ukomo wa mashindano yote ya maneno ni kiapo, kwa kuyathibitisha. Katika neno hili Yahweh akitaka kuwaonyesha zaidi sana warithio ile ahadi, jinsi mashauri yake yasivyoweza kubadilika, alitia kiapo katikati; ili kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo Yahweh hawezi kusema uongo, tupate faraja iliyo imara, sisi tuliokimbilia kuyashika matumaini yale yawekwayo mbele yetu; tuliyo nayo kama nanga ya roho, yenye salama, na nguvu, yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia, alimoingia Messiah kwa ajili yetu, mtangulizi wetu, amekuwa kuhani mkuu hata milele kwa mfano wa Melkizedeki."*** (Waebrania 6:16-20).

Basi tuamini ujumbe wa Maandiko Matakatifu na kuishi kwa kila neno ambalo linatoka kinywani mwa Yahweh (Mathayo 4:4, Luka 4:4, na Kumbukumbu la Torati 8:3). Kisha tutaruhusiwa kuingia kwenye Ufalme unaokuja wa Yahweh, Yahshua anaporudi. SNB

*Sacred Name Broadcaster*
*Bethel, PA 19507*

**PERIODICAL**

Reading, PA

# WMLK Radio

## Assemblies of Yahweh Shortwave

**Now Broadcasting 6 DAYS A WEEK**

**15150 kHz 1200-1700 GMT (7 AM - 12 PM EST)**

**17525 kHz 1730-2230 GMT (12:30 PM - 5:30 PM EST)**

**9275 kHz 2300-0400 GMT (6 PM - 11 PM EST)**

**On the air 24/7 at WMLKRadio.com, on TuneIn.com or at station.voscast.com/5cfe89883c143**

(Note: There are times that WMLK is not broadcasting because of maintenance or repairs.)




**New Frequencies and Times!**